



# COLLEGE OF YOUTH EDUCATION IN TANZANIA (CoYETa)



S.L.P 11836 MLANGO MMOJA MWANZA -TANZANIA  
[SIMU:+255\(028\)2540305](tel:+2550282540305), +255753188061, +255687231447 FAKSI: +255(028)2540305,  
Barua pepe: [info@coyeta.ac.tz](mailto:info@coyeta.ac.tz) or [coyeta@gmail.com](mailto:coyeta@gmail.com), Tovuti: [www.coyetamyc.ac.tz](http://www.coyetamyc.ac.tz)

## FOMU YA MAELEZO YA KUJIUNGA NA MASOMO KATIKA NGAZI YA STASHAHADA (ORDINARY DIPLOMA) KWA MWAKA WA MASOMO 2020/2021



Mkuu wa Chuo (CoYETa) anayo furaha kubwa kukuarifu ndugu,

kwamba kwa ufaulu ulioupata katika matokeo yako ya kidato cha nne 2019/2020, una fursa ya kujiunga na Masomo ya **STASHAHADA YA UTAWALA WA BIASHARA (ORDINARY DIPLOMA IN BUSINESS ADMINISTRATION)**, kwa miaka mitatu, katika chuo cha CoYETa kwa Muhula wa masomo utakaoanza tarehe 02/11/2020. Hivyo, unaombwa kufika shuleni kwako \_\_\_\_\_ au chuoni (CoYETa) kwa ajili ya maelezo zaidi na kuchukua fomu ya maombi. Chuo chetu kinatambulika na Serikali kwa **USAJILI WA KUDUMU wa nambari REG/BTP/007**

### 1. TAREHE YA USAJILI NA KUENZA MASOMO

Kwa kuwa usajili wa wanafunzi unazingatia taratibu za chuo (CoYETa) na maelekezo ya serikali (NACTE), unaombwa kufika chuoni au kuwasiliana na Afisa Usajili wa Chuo kabla ya tarehe **15/09/2020** kwa ajili ya kukamilisha taratibu hizo. Unapaswa kulipoti chuoni tarehe **20/11/2020** kwa ajili ya mhula wa masomo utakaoanza tarehe **02/11/2020**. Chuo chetu kipo Jijini Mwanza maeneo ya Mlango mmoja, Jengo la Vijana.

Matakwa ya kusajiliwa ni pamoja na:

- Kukamilisha malipo ya Usajili (NACTE) ambayo ni kiasi cha Tshs 20,000 (ishirini elfu) na malipo ya fomu ya kujiunga kiasi cha Tshs 10,000. Kiasi hicho cha fedha (Tshs 30,000) kinapaswa kulipwa kabla ya tarehe 15/09/2020.
- Kuwasilisha taarifa mhimu kwa ajili ya usajili ikiwa ni pamoja na vielelezo vya elimu yake (vyeti halisi vya shule, nakala za matokeo); na cheti cha kuzaliwa (kama anacho).
- Hakutakuwa na ubadilishaji wa majina yaliyopo kwenye vyeti vitakavyokuwa vimewasilishwa wakati wa zoezi la usajili isipokuwa imesemwa vinginevyo.

### 2. ADA YA KOZI

Chuo chetu kinatoza ada nafuu zaidi miongoni mwa vyuo vingi vya binafsi na serikali vinavyotoa kozi hii. Ada inaweza kulipwa kwa mara moja au kwa awamu zisizozidi nne(4) kulingana na uwezo wa mlipaji kama inavyooneshwa katika jedwali hapa chini:

#### A: Mgawanyo wa Ada kwa Mwaka wa Kwanza ni Kama Ifuatavyo:

<b>Jina la Kozi : Stashahada ya Utawala wa Biashara</b>	
<b>Kitu kinacholipiwa</b>	<b>Kiasi (Tshs)</b>
Ada ya Kozi	710,000
Ada ya Uthibiti Ubora (NACTE)	15,000
Fomu ya Kujiunga	10,000
Kitambulisho cha mwanafunzi	5,000
Mchango wa Serikali ya Wanafunzi	5,000
Huduma ya Kwanza	5,000
Mahafali	20,000
Ada ya Mtihani	50,000
Stationeries	40,000
Ada ya Usajili	40,000
<b>Jumla Kuu</b>	<b>900,000</b>

<b>Awamu Za Kulipa</b>			
<b>S/N</b>	<b>AWAMU</b>	<b>MUDA WA MWISHO WA KULIPA</b>	<b>KIASI (TSHS)</b>
1	Awamu Ya Kwanza	02 Novemba 2020	300,000
2	Awamu Ya Pili	02 Februari 2021	200,000
3	Awamu Ya Tatu	02 Mei 2021	200,000
4	Awamu Ya Nne	02 Agosti 2021	200,000
<b>Jumla</b>			<b>900,000</b>

**B: Mgawanyo wa Ada kwa Mwaka wa Pili na wa Tatu ni Kama Ifuatavyo:**

<b>Jina la Kozi : Stashahada ya Utawala wa Biashara</b>	
<b>Kitu kinacholipiwa</b>	<b>Kiasi (Tshs)</b>
Ada ya Kozi	810,000
Ada ya Uthibiti Ubora (NACTE)	15,000
Fomu ya Kujiunga	10,000
Kitambulisho cha mwanafunzi	5,000
Mchango wa Serikali ya Wanafunzi	5,000
Huduma ya Kwanza	5,000
Mahafali	20,000
Ada ya Mtihani	50,000
Stationeries	40,000
Ada ya Usajili	40,000
<b>Jumla Kuu</b>	<b>1,000,000</b>

**NAMNA YA KULIPA**

- i) Fedha zote kwa ajili ya gharama za masomo (ada, hosteli, n.k) italipwa katika Benki ya CRDB hapa chuoni kupitia FAHARI HUDUMA au Kwa kupitia tawi lolote la **Benki ya CRDB**, kwenye Akaunti nambari **0150355105000** kwa jina la **College of Youth Education in Tanzania**.
- ii) Mwanafunzi anapaswa kuwasilisha Nakala Halisi ya Malipo (Original Bank Pay in Slip) kwenye ofisi ya Uhasibu Chuoni. Hundi, Keshi, na aina nyingine za malipo hazitapokelewa.
- iii) Ada haitarudishwa kama mwanafunzi amesitisha maosomo au ameacha chuo.

**3. PICHA (PASSPORT SIZE)**

Mwanafunzi anatakiwa kuja na picha nne za passport, moja kwa ajili ya kitambulisho cha chuo na nyingine kwa ajili ya matumizi ya ofisi.

**5. HUDUMA YA MALAZI, CHAKULA, NA MATIBABU**

- i) Chuo kina hosteli nzuri na za kisasa kwa wanafunzi wa mbali au wanaohitaji. Gharama za hostel ni shilingi laki nne (Tshs 400,000/=) kwa mwaka, fedha hii italipwa kwa awamu mbili. Gharama hizo zinajumuisha chumba, kitanda, godoro, umeme, na maji.

- ii) Chuo hakitoi chakula kwa wanafunzi, hivyo mwanafunzi anaruhusiwa kujiandalia chakula chake katika jiko lililo ndani ya hosteli. Pia, kwa mwanafunzi ambaye hawezi kupika anaweza kupata chakula maeneo ya karibu na chuo/hosteli kwa gharama nafuu kabisa.
- iii) Gharama za matibabu ni juu ya wanafunzi wenyewe. Hata hivyo, chuo kinaweza kutoa huduma ya kwanza kwa mwanafunzi anapopatwa na maradhi huku jitihada za kumjulisha mzazi/mlezi zikiendelea.
- iv) Chuo kinayo maktaba yenye vitabu vizuri na maabara ya sayansi na computer kwa ajili ya wanafunzi. Hata hivyo, chuo hakiwajibiki kumnunulia mwanafunzi vifaa vyake binafsi vya kujifunzia kama kikokotozi, nk.

## **6. MAWASILIANO**

Wanafunzi waliosajiliwa chuoni kwetu wanapaswa kutembelea mara kwa mara mbao za matangazo na tovuti yetu kwa ajili ya kupata taarifa mbalimbali za kitaaluma na mambo mengine ya kijamii kama ratiba za masomo, matokeo ya mitihani, semina, n.k

## **7. NIDHAMU**

Wanafunzi wote wanatakiwa kuonesha tabia njema ndani na nje ya maeneo ya chuo, hii ikiwa ni pamoja na kufuata sheria na taratibu zote za chuo. Kushindwa kufanya hivyo, kutasababisha mhusika kuchukuliwa hatua za kinidhamu ambazo zinaweza kuwa ni pamoja na kufukuzwa chuo.

**NB: SAMBAMBA NA KOZI YA UHASIBU, MANUNUZI & UGAVI, NA UTAWALA WA BIASHARA, CHUO KWA KUSHIRIKIANA NA CHUO MAMA CHA MWANZA YOUTH CENTRE (MYC) KINATOA KOZI NYINGINE MBALIMBALI KAMA KOZI YA MAABARA (LABORATORY ASSISTANT), UTALII, USAFIRI WA ANGA, HOTELI, UHAZILI (SECRETARIAL), MUZIKI, KINGEREZA NA KIFARANSI, COMPUTER APPLICATIONS & MAINTENANCE. HIVYO, CHUO KINAKUPA FURSA YA KUBADILISHA KOZI NA KUSOMA KOZI NYINGINE YOYOTE INAYOTOLEWA NA CHUO CHETU KULINGANA NA MAHITAJI YAKO.**

**IMETOLEWA NA:**

Ev. Emmanuel Mambo  
(Mkuu wa Chuo)

**KARIBU SANA CoYETa UFANIKIWE KIELIMU, KIROHO NA KIMWILI**

***Kwa msaada zaidi piga kwenye namba 0687231447 au 0768385986***